**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU TAARIFA YA SERIKALI JUU YA HALI YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUHUISHA UCHUMI NA HUDUMA ZA JAMII KUPITIA FEDHA ZA AHUWENI YA UVIKO 19 KUTOKA SHIRIKA LA FEDHA ZA DUNIA (IMF)

---

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kufika hapa katika Mkutano huu wa Nne wa Baraza la Kumi katika hali ya amani na utulivu na kuweza kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia, inatoa shukurani zake za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kufanikisha upatikanaji wa fedha za Kuhuisha Uchumi Na

Huduma za Jamii kupitia Fedha za Ahuweni ya Uviko 19 kutoka Shirika La Fedha Za Dunia na maelekezo ya namna ya kuzitumia. Kwa hakika miongozo na maelekezo yao yamekuwa na tija kubwa katika kufanikisha utekelezaji wa miradi mbali mbali ndani ya nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa uwezo, ujasiri, hekima na busara katika uongozi wao ili azma yao ya kuwatumikia na kuwaletea maendeleo wananchi ifikiwe kwa wakati waliokusudia.

Mheshimiwa Spika, vile vile, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kukidhi matakwa ya kanuni ya *44(3)* ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la *2020* ya kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Taarifa ya Serikali juu ya hali ya Utekelezaji wa Programu ya Kuhuisha Uchumi Na Huduma za Jamii kupitia Fedha za Ahuweni ya Uviko 19 kutoka Shirika La Fedha Za Dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwatambulisha Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | M/ Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| 9. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 10. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani. |

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilikutana na kuijadili Taarifa hii kwa kuipitia ukurasa kwa ukurasa na kutoa maoni yake juu ya kila hatua ambayo imeona ni vyema kufanya hivyo ili kujenga na kufikia dhamira njema ambayo Serikali yetu imekusudia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa azma ya Serikali ni njema na inaleta matumaini chanya kwa mwananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla juu ya matumizi ya fedha hizo, Kamati yetu inapata wasiwasi kupitia malengo yaliyowekwa katika *ukurasa wa tatu* wa Taarifa hii kwamba malengo haya hayatafikiwa ya

kukamilisha miradi ndani ya kipindi kilichopangwa kutokana na muda wenyewe kuwa mfupi mno na tukizingatia baadhi ya miradi ipo katika hatua za awali sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inahisi iwapo Serikali itafuata moja kwa moja Sheria ya Manunuzi katika utekelezaji wa miradi ya fedha hizo basi haitoenda sambamba na kipindi kilichowekwa cha matumizi ya fedha za miradi hii. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Manunuzi ambayo utekelezaji wake katika masuala mengi yanaonekana kuchukua muda mrefu na pia ndiyo sababu ya kuchelewa miradi hii. Aidha Kamati yangu inaomba Serikali  kutafuta utaratibu maalumu ambao utasaidia kuzitumia fedha hizo kwa haraka kama vile (force Account) kama ilivyo kwa wenzetu wa Tanzania Bara ambao kwa asilimia kubwa wameshakamilisha miradi yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imebaini kukosekana kwa viwango vya ubora wa miradi ya ujenzi inayotekelezwa kupitia fedha hizi katika maeneo mbali mbali ya Sekta ya Elimu na Afya, mbali ya kuwepo kwa Mshauri Elekezi ambaye ni Wakala wa Majengo Zanzibar lakini miradi haioneshi ubora na kazi zinafanywa kwa kuripua ili kwenda sambamba na muda uliowekwa. Kamati inashauri Serikali kupitia Kamati zake Tatu ambazo imeziunda kusimamia miradi hii kufuatia kikamilifu kila

sehemu na kwa kila mradi ili kujiridhisha na mradi husika na Kamati zisisite kuwachukulia hatua wale wote ambao watakua chini ya viwango vinavyo tarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa Miradi ambayo imeelezwa vyema kuanzia *Ukurasa wa Nne*, Kamati yangu imebaini na inapata wasiwasi kuona kwamba mpaka sasa ni muda mrefu umepita tangu fedha hizi kutolewa na Zanzibar hatujafikia hata robo katika hatua ya utekelezaji wake na muda ulioabakia katika utekelezaji wa Bajeti ya 2021/2022 ni miezi mitatu, je Serikali itakamilisha vipi miradi hii ambayo kwa kiasi kikubwa sana ipo katika hatua za awali katika ujenzi wake na mengine bado haijaanza.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia, katika *ukurasa wa Tano* inaiyomba Serikali kuwashirikisha kikamilifu wananchi na viongozi wa maeneo yenye miradi hii hususan katika Majimbo ambayo yameguswa na miradi ya ujenzi ya sekta ya elimu, afya, maji na umeme, kwani Kamati inaamini ushirikishwaji wa jamii na viongozi katika ngazi za Majimbo, Wadi na Shehia haupo au sio rafiki na miradi iliyopelekwa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, Kupitia Ukurasa wa Sita wa Taarifa hii, kwa

faida ya Baraza hili Tukufu na wananchi kwa ujumla, Kamati imebaini juu ya Fedha za Tanzania Shilingi *Bilioni Mbili, Milioni Mia Saba Sabiini na Nne* (2,774,000,000/=) zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa Jengo la Bweleo, maelezo yake hayatoshelezi. Kamati inataka kujua hasa ukizingatia Fedha hizi ni za kazi maalumu kwamba, Jengo hili linamilikiwa na nani, limelenga kutumiwa kwa madhumuni gani na taratibu zilizotumika kujua thamani halisi ya bei itakayonunuliwa. Aidha, Kamati inahoji juu ya umuhimu wa kununua jengo kwa kutumia Fedha hizi ambazo lengo lake lipo katika kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukarabati wa skuli 22 uliokusudiwa kufanywa kupitia fedha hizi utahusisha na zile zilizoundiwa Kamati Teule na Baraza hili Tukufu na kutolewa ripoti yake ndani ya Baraza hili bila ya kuwepo kwa utekelezaji wa maagizo ya kamati hiyo kwa muda mrefu kutokana na sababu mbali mbali, au zimeibuliwa Skuli nyengine tofauti na zile zilizofanyiwa uchunguzi wa awali.

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu wa kuzifanyia ukarabati mkubwa wa skuli 14 zenye hali mbaya Kamati yangu inasisitiza zaidi kujumuishwa na zile skuli ambazo ziliundiwa Kamati Teule iwapo hazimo katika orodha ya awali Aidha, Kamati inasisitiza

ukarabati huo uwe wa viwango na ubora mkubwa ambao hautapelekea kurejea umo kwa umo kukarabati majengo kwa mustakbali mzuri na ustawi bora wa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, Katika ukurasa wa Nane wa Taarifa hii, Kamati yangu imebaini juhudi za Serikali kwa kuwajali wanafunzi wake kwa kuanzisha utaratibu wa kutengeneza madawati kupitia mafundi wazalendo. Hata hivyo, Kamati inashauri utaratibu uliotumika katika ujenzi wa madarasa pia utumike katika kuwapata mafundi hawa ambao itakuwa mara yao ya kwanza katika kutekeleza miradi ya Serikali. Aidha kamati inasisitiza madawati haya yatengenezwe ndani ya nchi na kwa kiwango kilicho bora kama ripoti ilivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya, Kamati yangu imebaini katika *ukurasa wa 10* sehemu ambayo imetengewa Shilingi Milioni Mia Tatu Kumi na Mbili (312,000,000/=) kwa ajili ya kuimarisha huduma za damu salama ambapo Serikali itanunua majokofu manne (4) ya kuhifadhia damu na vifaa vya kukusanyia damu, Kamati yangu inashauri vifaa hivi pamoja na majokofu haya manne yagaiwe kwa Unguja na Pemba kama ilivyo utaratibu wa vifaa vyengine kwani Pemba kuna changamoto kubwa ya vifaa vilivyo bora vya uhifadhi wa damu salama kwa matumizi ya

wagonjwa waliopo katika hospitali zetu mbali mbali hali inayosababisha kuharibika kwa damu salama ambayo ni muhimu kwa maisha ya watu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Maji. Kamati yangu kupitia ukurasa wa Kumi na Tatu imepitia nakuona kiasi kikubwa cha fedha zilizotengwa kiasi cha fedha Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Saba Themanini na Moja, Laki Sita na Sitini Elfu (6,781,660,000/=) zilizotengwa kwa ajili ya Ununuzi wa Mashine za Maji kwa upande wa Unguja na Pemba. Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwaondolea wananchi wake tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama, hata hivyo, Kamati inaiomba Serikali ifatilie kwa ukaribu zaidi utekelezaji wa mradi huu ili kukidhi vigezo na ubora wa pampu zote zitakazo nunuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, imebaini kuwepo kwa uharibifu mkubwa na uchakavu wa miundo mbinu ya maji kama mabomba ambayo yanayovuja mara kwa mara na yasio na viwango. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Wizara kuzingatia ubora wa mabomba yatakayonunuliwa kupitia mpango huu kwani yapo mabomba ambayo hayana ubora na husababisha kupasuka kila siku na hivyo kupotea kwa maji katika sehemu mbali mbali za

Zanzibar na hatimae kutokea kwa maradhi ya kipindupindu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Nishati ya Umeme Kamati imebaini ndani ya Zanzibar kuna ukatikaji wa umeme mara kwa mara ambao husababisha vitu vya wananchi kuharibika. Hivyo, Kamati inashauri fedha hizo zitumike ipasavyo kwa kutekeleza vyema agizo la Muheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi la kuwataka wananchi wasinunue nguzo za umeme pamoja na kufuata mipango ya Serikali katika kuboresha huduma za nishati ya umeme kwani malengo yake ni bora na ni yenye kujenga maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kamati yangu inaunga mkono mpango uliowekwa wa kuwasaidia wananchi kujikwamua na hali ngumu ya kimaisha iliyosababishwa na athari za UVIKO 19 na hivyo kupelekea kushuka kwa kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika *ukurasa wa 17* wa Taarifa hii ambayo imetengwa kiasi cha Shilingi Bilioni Ishirini na Nane, Milioni Mia Nane Arobaini na Tano, Laki Nne na Arobaini Elfu (28,845,440,000/=) zimetengwa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia shughuli za Uchumi wa Buluu

ikijumuisha ununuzi wa boti mia tano sabiini na saba (577) za mita nane (8) na boti mia tano (500) za mita tano (5) na kuwasaidia wajasiriamali wanaoanika na kuchakata madagaa, Kamati inashauri ugawaji wa boti hizi uzingatie maeneo yenye uhitaji.

**Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Kamati inaiomba Serikali kununuwa boti zilizobora na za uhakika  kwa kuangalia suala zima la bei na zabuni kutokana na uzoefu unaonesha sehemu hii ndipo ubadhirifu unapotokea. Aidha, tunasisitiza kuangalia pia matumizi yaliyokusudiwa kwa kutolewa elimu ya kutosha ya utumiaji wa boti hizo sambamba na kuwatafutia wananchi vifaa vya kileo vya uvuvi kama “fish finder” ili wananchi hao waweze kuvua kwa uhakika.

**Mheshimiwa Spika,** katika mradi wa Ufugaji wa Nyuki ambao umetengewa kiasi cha Shilingi Milioni Mia Tisa na Sitini (960,000,000/=) kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake katika ufugaji wa nyuki. Kamati inashauri kutokana na uzoefu wa miradi mingi kama hii ya ufugaji wa nyuki na mengineyo inakosa usimamizi na utaalamu ambao utapelekea kuendelea na kuleta mafanikio. Matokeo yake miradi mingi hufa kama vile miradi ya JK na AK na fedha nyingi hupotea bila ya kuwepo mafanikio

yoyote kwa jamii na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia ripoti hii kamati pia inaiomba kujua ujenzi wa tanuri la kuanikia madagaa kule Fungu Refu Mkoa wa Kaskani Unguja, ambao ulitajwa katika Bajeti iliyopita tulielezwa Kamati inapenda kujua mpango ule umefikia wapi na iwapo utazihusisha fedha hizi katika utekelezaji wake kwani jambo lile ni jema kwa maendeleo chanya ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii na nawaomba Wajumbe wa Baraza hili kutoa michango yao juu ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba Kuwasilisha.

..................................

*(Hassan Khamis Hafidh)*

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI.

ZANZIBAR